

## **FORMULA YA KUKU CHOTARA**

Utengenezaji wa chakula cha kuku kwa kutumia Formula sahihi ni njia nzuri kwa mfugaji kwa kupunguza gharama za mradi wake wa kuku, pia kuhakikisha chakula kinakua na virutubisho muhimu kwa usahihi.

Ifuatayo ni formula ya utengenezaji wa chakula cha Kuku, Starter, grower na Finisher.

### **1. CHICKS STARTER MASH , WIKI 1 - 7**

- Pumba za mahindi 15kg
- Mahindi paraza size ndogo 45kg
- Daga/Soya 10kg
- Mashudu ya pamba 8kg
- Mashudu ya alizeti 10kg
- Chumvi 0.5kg
- Unga wa mifupa 8kg
- Methionine 0.25kg
- Premix 1kg
- Lysine 0.1kg
- DCP 2KG
- Chokaa 8kg
- Toxin binder 0.1kg

**Inatakiwa isikugharimu zaidi ya 90k ikizidi nipe taarifa nirekebishe kutokana na malighafi ulizo nazo karibu.**

**GROWER MASH, WIKI 8- 18(watakapo anza kutaga)**

Mahindi yaliyo parazwa saizi ya kati 43kg

Pumba ya mahindi 40kg

Mashudu ya alizeti 20kg

Dagaa/Soya 20kg

DCP 2kg

Unga wa mifupa 9kg

Chokaa 6kg

Chumvi 0.5kg

Premix 1kg

Methionine 0.1 kg

Lysine 0.1 kg

Toxin binder 0.1kg

**Gharama ya kutengeneza isizidi 120000**

**NB: Chakula hiki kilishwe mpaka pale utakapo okota yai la kwanza bandani.**

**LAYERS MASH WIKI 18 ( wakianza kutaga nakuendelea mpaka kuuza kuku wako)**

Mashudu ya alizeti 15kg

Pumba za mahindi 30kg

Mahindi paraza saizi kubwa 55kg

Chokaa 9kg

Soya/ Dagaa walio sagwa 20 kg

Unga wa mifupa 9kg

Layer premix 1kg

GLP 0.5kg

DCP 2 Kg

Chumvi 0.5kg

Egg booster 1kg (Wanapo anza kutaga mwezi mmoja wa kwanza kisha acha kuitumia).

Methionine 0.15kg

Lysine 0.15 kg

Toxin binder 0.2kg

Carogold / Chrolophill yellow 0.2kg

**Gharama isizidi 120000**

## **MUHIMU**

- Hakikisha unachanganya vizuri ili kupata mchanganyiko wenyewe uwiano Sahihi wa virutubisho.
- Chakula kihifadhiwe vizuri kuzuia unyevu.
- Kuku wapewe chakula kwa kiasi kulingana na umri na idadi yao.
- Maji yawepo muda wote
- Kuku wakianza kutaga wapewe masaa 16 ya mwanga